

KISWAHILI NA UTAFITI

VYUO VIKUU NA MAENDELEO YA KISWAHILI: MCHANGO WA TASNIFU ZA UZAMILI NA UZAMIFU KATIKA IDARA ZA KISWAHILI

Magdaline Nakhumicha Wafula

Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret

Ikisiri

Kiswahili ni miongoni mwa lugha maarufu ulimwenguni kutokana na matumizi yake mapana. Aidha, kimepata hadhi ya kuwa lugha ya kimataifa kutokana na ukwasi wake kimsamiati, kiistilahi na kimaandishi. Ongezeko la wataalamu na watafiti wa lugha hii hasa katika vyuo vikuu limechangia hali hii pakubwa. Hii leo walimu wengi nchini Kenya wanaofunza somo la Kiswahili katika shule za upili na vyuo vya ualimu wana shahada ya kwanza au hata ya pili katika taaluma ya Kiswahili. Aidha, idadi ya wanafunzi wanaochukua shahada za uzamili na uzamifu katika vyuo vikuu barani Afrika na kwingineko imeongezeka. Mojawapo ya sifa bainfu za chuo kikuu ni msistizo wa utafiti katika taaluma yoyote ile. Hali hii inadhihirika zaidi katika viwango vya uzamili na uzamifu. Mathalan katika taaluma ya Kiswahili na fasihi yake, baadhi ya mahitaji kwa wazamili na wazamifu ni kutafitia mada maalum na kuandika tasnifu kwa Kiswahili. Katika makala hii ninaangazia namna mahitaji haya yamechangia katika maendeleo ya Kiswahili na fasihi yake. Tasnifu kadhaa za uzamili na uzamifu katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Moi-Eldoret zinarejelewa. Mada, matokeo na mapendekezo ya tasnifu anuwai za kabla na baada ya mwaka 1984 zinajadiliwa kiulinganishi. Mwaka wa 1984 ni muhimu nchini Kenya ni wakati ambapo mapendekezo ya Tume ya Mackay kukifanya Kiswahili somo la lazima katika shule za msingi na za upili katika mfumo wa elimu wa 8-4-4 yalianza kutekelezwa. Makala hii inaonyesha jinsi jitihada za makusudi za serikali kuhusu sera ya lugha na elimu nchini Kenya zimekiinua na kukiendeleza Kiswahili.